

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخَلَفَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يُكِنْنَ هُمْ دِينَهُمُ الَّذِي أَرْضَى لَهُمْ وَلَمْ يُبَدِّلُنَّهُمْ فَإِنَّمَا يَعْذِذُونَ
يَعْذِذُونَ لَا يَشْرِكُونَ بِهِ شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ



Jumamosi, 28 Muharram 1446 H

03/08/2024 M

Na: HTS 1446 / 05

Taarifa ya Habari

Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan Yaandaa Maandamano mjini Al-Qadarif Kutaka Kukomeshwa kwa Vita na Umwagaji damu ya Waislamu (Imetafsiriwa)

Mnamo siku ya Ijumaa, Agosti 2, 2024, Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan iliandaa maandamano katika mji wa Al-Qadarif baada swala ya Juma'a karibu na Jami' Al-Atiq (Msikiti Mkongwe) katika Soko la Al-Qadarif. Maandamano hayo yalitaka kukomeshwa kwa vita na umwagaji damu ya Waislamu, na kuuangaza Ummah kuhusu uhalisia wa njama za Magharibi zinazoongozwa na Marekani na Ulaya za kutaka kudhibiti mamlaka yao. Maandamano hayo yaliwataka wenye ikhlasi kushikamana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu badala ya matakwa ya Kafiri Magharibi.

Mashababu walibeba mabango yenye maandishi yanayosomeka:

1. Hizb ut Tahrir inatoa wito wa kukomesha vita na uwajibikaji kwa wale wanaokula njama dhidi ya watu wetu nchini Sudan.
2. "Iwapo Waislamu wawili watakutana na panga zao, muuaji na aliyeuawa wote wamo Motoni."
3. Komesheni uingiliaji wa Marekani katika ardhi za Kiislamu kwa kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume.
4. Khilafah inalinda ardhi na kulinda heshima; isimamisheni enyi Waislamu.
5. Komesheni vita kwa kumtii Rahman, sio matakwa ya Wamarekani.
6. Maadui wa Uislamu wasingechechea vita kati ya Waislamu lau kama Waislamu wangekuwa na Khalifa.
7. Kuangamia kwa Al-Kaaba jiwe kwa jiwe ni sahali kwa Mwenyezi Mungu kuliko tone la damu ya Muislamu.
8. Lau sio kwa ushirika wa watawala, damu tukufu isingemwagika; kwa Khilafah, damu ya Waislamu inalindwa.
9. Vita vya Sudan ni vita vya kung'ang'ania madaraka kati ya Marekani na Ulaya, na wahanga ni watu wa Sudan.

Watu wetu katika mji wa Al-Qadarif waliingiliana na maandamano hayo na wakasifu juhud za Mashababu wa Hizb, wakiomba ushindi na uthabiti wa Hizb.

Ibrahim Othman (Abu Khalil)
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Sudan